

# HALMASHAURI YA MJI KASULU



SimuNa. +255 28 2810355

Tovuti: [www.kasulutc.go.tz](http://www.kasulutc.go.tz)

Email: [td@kasulutc.go.tz](mailto:td@kasulutc.go.tz)

S.L.P 475

**KASULU**

5/4/2018

## TANGAZO LA KAZI

Halmashauri ya Mji wa Kasulu inawatangazia nafasi ya kazi. Lengo la kutangaza nafasi hizi ni kuimarisha utendaji kazi katika Halmashauri ya Mji Kasulu. Nafasi zinazotangazwa ni kama ifuatavyo;

### 1. Mtendaji wa Mtaa III (Nafasi 13)

#### Sifa za Mwombaji

- i. Cheti cha kidato cha IV au VI
- ii. Aliliyehitimu mafunzo ya Astashahada/ cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kunachotambulika na Serikali.

#### Kazi za kufanya:-

- i. Mratibu na utekelezaji wa sera na sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika mtaa
- ii. Mshauri wa kamati ya mtaa kuhusu mipango ya maendeleo katika mtaa
- iii. Msimamizi wa utekelezaji wa sheria ndogo pamoja na sheria zinazotumika katika mtaa
- iv. Mshauri wa kamati ya mtaa kuhusu masuala ya ulinzi na usalama
- v. Msimamizi wa utekelezaji wa mkakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umasikini katika mtaa

- vi. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote
- vii. Kuandaa ma kutunza rejesta ya wakazi wote wa mtaa
- viii. Na atawajibika kwa mtendaji wa kata

## **Mshahara: Ngazi ya TGS B**

### **Muda wa kazi**

Kazi hii inatarajiwa kuwa chini ya masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni

## **2. Dereva II (Nafasi 1)**

### **Sifa za Mwombaji**

- (i) Awe Mtanzania
- (ii) Cheti cha kidato cha IV
- (iii) Awe na leseni daraja la "E" au "C1" ya uendeshaji wa magari ambayo amafanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali
- (iv) Awe amahudhuria Mafunzo ya Msingi ya uendeshaji Magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na serikali
- (v) Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi daraja la II, watafikiriwa kwanza.



### **Kazi za kufanya:-**

- (i) Kuendesha magari ya abiria, na malori,
- (ii) Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote, na kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo,
- (iii) Kufanya matengenezo madogo madogo katika gari,
- (iv) Kutunza na kuandika daftari ya safari "Log-book" kwa safari zote.
- (v) Na kazi nyingine atakazopangiwa na msimamizi wake.
- (vi)

### **Mshahara: Ngazi ya TGS B**

#### **Muda wa kazi**

Kazi hii inatarajiwa kuwa chini ya masharti kudumu na malipo ya uzeeni.

### **3. Muhudumu wa jikoni II (Nafasi 1)**

#### **Sifa za Mwombaji**

- (i) Awe mtanzania
- (ii) Cheti cha kidato cha IV
- (iii) Cheti cha mafunzo ya uhudumu wa jikoni kutoka vyuo vinavyotambulika na Serikali

### **Kazi za kufanya:-**

- (i) Kusafisha vyombo vya kupikia
- (ii) Kusafisha vyombo vya kulia chakula
- (iii) Kusafisha sehemu ya kulia chakula
- (iv) Kuwatayarishia wapishi/waandazi vifaa vya kazi
- (v) Kusafisha maeneo ya kupikia
- (vi) Na kazi nyingine atakazopangiwa na msimamizi wake.

**Mshahara: Ngazi ya TGOS A**

**Muda wa kazi**

Kazi hii inatarajiwa kuwa chini ya masharti ya kudumu (Operational Services)

**Namna ya kuwasilisha maombi:-**

(i) Maombi yote yaambatanishwe na maelezo binafsi (CV), Nakala ya Vyeti vya Elimu vilivyothibitishwa kisheria (Certified) na mafunzo ya Kompyuta.

(ii) Maombi yawasilishwe kwa njia ya barua na yatumwe kwa Mkurugenzi wa Mji, Halmashauri ya Mji wa Kasulu, S.L.P 475 Kasulu.

(iii) **Mwisho wa kupokea maombi** ni tarehe 19/04/2018

**Tambili:** Wananchi wanaoshi katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu wanahimizwa kutuma maombi yao.

Imetolewa na:



Fatina H. Laay

**MKURUGENZI WA MJI**

**HALMASHAURI YA MJI**

**KASULU.**

**MKURUGENZI WA MJI  
HALMASHAURI YA MJI WA KASULU**

**Nakala:** Ofisi za Watendaji wa Kata zote

**"Mbao zote za matangazo"  
Halmashauri ya Mji Kasulu**